



**CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU
NYERERE**



**KONGAMANO MAALUMU LA KITAALUMA LA KUMBUKIZI YA MWALIMU JULIUS K.
NYERERE LITAKALOFANYIKA TAREHE 10 OKTOBA 2024 KATIKA CHUO CHA
KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE-KAMPASI YA KIVUKONI**

Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere anapenda kuwaalika Viongozi na Wananchi mbalimbali kushiriki katika Kongamano Maalumu la Kitaaluma litakalofanyika siku ya Alhamisi Tarehe 10 mwezi wa Kumi, mwaka 2024 katika ukumbi wa **PROF.COLIN LEYS** kampasi ya Kivukoni, Jijini Dar es Salaam.

Kongamano hilo litakuwa na **MADA KUU** isemayo: “**MAONO YA MWALIMU NYERERE KATIKA UONGOZI NA MAENDELEO ENDELEVU**”. (The Legacy of Mwalimu Nyerere in Leadership and Sustainable Development).

Lengo la Kongamano hilo ni kumuenzi Baba wa Taifa katika mambo aliyopigania na kuyasimamia.

Mada ndogo Nne zitawasilishwa katika kongamano hilo kama ifuatavyo:

1. Falsafa ya Mwalimu Nyerere ya Kujitegemea na Maendeleo Endelevu ya kisasa.
2. Uongozi na Utawala wa Mwalimu Nyerere kuhusu Mfumo wa Maadili kwa Maendeleo Endelevu
3. Urithi wa Mwalimu Nyerere Katika Mageuzi ya Kielimu na Maendeleo endelevu
4. Falsafa au Maono ya Mwalimu Nyerere katika Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo ya Jamii.

Mgeni Rasmi wa Kongamano hilo ni **MHE. STEPHEN MASATO WASSIRA**.

IMETOLEWA NA:

KITENGO CHA MAWASILIANO NA MASOKO-MNMA

2.10.2024

NYOTE MNAKARIBISHWA KATIKA KONGAMANO HILI